**CHUO CHA UFUNDI ARUSHA KWA KUSHIRIKIANA NA KOICA WAZINDUA MAABARA YA UBUNIFU IDARA YA UHANDISI MITAMBO.**

Na mwandishi wetu, Arusha .



*Mkurugenzi Mkazi wa KOICA Bwa. Manshik Shin (wa pili kushoto) akikata utepe kuashiria ufunguzi wa Maabara ya Ufundi Mitambo Kielektroniki. Kushoto kwake ni Mkuu wa Chuo cha Ufundi Arusha Prof. Musa Chacha.*

Chuo cha ufundi Arusha (ATC) kwa kushirikiana na Wakala wa Ushirikiano wa Kimataifa kutoka Korea yaani Korea International Cooperation Agency (KOICA) wamezindua rasmi maabara ya ubunifu ya idara ya uhandisi mitambo itakayowasaidia wanafunzi kujifunza kwa ufanisi mkubwa kwa kutumia teknolojia za kisasa.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo chuoni hapo ,Mkuu wa chuo cha ufundi Arusha, Prof. Musa Chacha amesema kuwa ufunguzi wa maabara hiyo una faida kubwa sana kwani ina vifaa vya kisasa vya kufundishia wanafunzi pamoja na vile vya kubuni michoro mbalimbali kwa kutumia ufundi wa hali ya juu.

Aidha amesema kuwa ,mradi huo una thamani ya dola za Marekani 28 ,000 ambapo kati ya hizo chuo kimechangia dola 4,000 .

Amesema kuwa , maabara hiyo ina vifaa vya kisasa ambavyo vinafundisha wanafunzi jinsi ya kubuni michoro mbalimbali kwa njia za kisasa kwa kutumia kompyuta za hali ya juu pamoja na 'printer' ambazo zinachora vitu kwa kisasa zaidi .

Dokta Chacha amesema kuwa uhusiano kati ya chuo cha ufundi Arusha na Korea ulianza siku nyingi na kipindi cha mwanzoni walipata mradi mkubwa ambao kazi kubwa ilikuwa ni kuanzisha mafunzo ya Programu ya Uhandisi Mitambo kielektroniki (Mechatronics) ambayo ilikua na lengo la kuandaa mafundi kwenda kufanya kazi kwenye viwanda ambavyo vinatumia teknolojia ya hali ya juu ambapo wanakaa na mitambo inafanya kazi na wao wanaielekeza kitu cha kufanya .

Aidha amesema kuwa, baada ya mradi huo kuendelea na kufanikiwa na kuona wanafunzi wanasoma sana ndipo wakaanza mkakati mwingine na wenzetu wa KOICA kwa kuwaleta watu wanaojitolea wenye uwezo mkubwa sana na umahiri mkubwa na kuja kufundisha walimu na wanafunzi .

Amesema kuwa, mwaka uliopita walipata mkufunzi mmoja wa kujitolea ambaye amekaa nao kwa muda wa miaka miwili sasa ambapo kupitia yeye wakapata mradi mwingine wa kuanzisha maabara ya kisasa, kwani ni maabara ya kwanza katika nchi ya Tanzania katika vyuo vya elimu.

"Tunaamini kwa kupitia maabara yetu vijana wetu wataweza kujifunza na kuandaa michoro mbalimbali ya vifaa ambavyo vinatumika na kuvitengeneza hivyo vifaa, tunatarajia mafanikio makubwa kupitia mradi huu."amesema Prof. Chacha .

Aidha amefafanua kuwa, maabara hiyo italeta mafanikio makubwa kwa vijana namna ya kuwafanya waweze kutengeneza vitu vinavyouzika na vyenye umahiri mkubwa na kuweza kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa popote watakapokuwa kwani wanapata umahiri wa kutengeneza michoro mbalimbali na kuiunda na kuweza kuiuza na hii ni mafanikio makubwa sana katika viwanda vyetu.

Mkurugenzi Mkazi wa KOICA Manshik Shin amesema kuwa maabara hiyo yenye uwezo wa kutengeneza muundo wa 3D kwa ufanisi wa mitambo ya

ubunifu itasaidia sana kuongeza ufanisi kwa wafanyakazi pamoja na wanafunzi katika utendaji kazi wao wa kila siku .

Amesema kuwa,kutendo hicho kinaashiria hatua muhimu mbele katika dhamira ya pamoja ya kuongeza ubora wa elimu ya ufundi nchini Tanzania na kuwezesha kizazi kijacho cha wahandisi, wabunifu, na wazalishaji.

"Ulimwengu unabadilika haraka,tunaishi katika wakati ambao teknolojia na uvumbuzi huendesha karibu kila nyanja ya maisha na kazi. Katika enzi hii ya dijiti, muundo wa 3D, modeli, na teknolojia za kuchapa sio zana tu, ni ujuzi muhimu.."amesema .

Shin ameongeza kuwa ,kutoka kwa muundo wa magari na utengenezaji hadi vifaa vya matibabu na suluhisho endelevu za nishati, teknolojia ya 3D iko kwenye moyo wa uhandisi wa kisasa na hii ndio sababu Koica ameshirikiana na ATC kuanzisha maabara ya muundo wa 3D wa kukata.

"Maabara hii ina kompyuta za hali ya juu, wachunguzi wakubwa, printa za 3D, na programu muhimu kama vile AutoCAD na SolidWorks pamoja na vifaa vya kufundishia vilivyosasishwa na vikao vya mafunzo vilivyojitolea kwa wanafunzi na waalimu."amesema .

Amesema kuwa ,zaidi ya wanafunzi 430, pamoja na idadi kubwa ya wanafunzi wa kike, sasa wanapata moja kwa moja kwenye kituo hiki. Hii ni karibu zaidi ya vifaa, ni juu ya fursa ambapo Wanafunzi katika uhandisi wa mitambo, mechatronics, na uhandisi wa vifaa sasa wataweza kutumia maarifa yao kwa wakati halisi, kupata uzoefu wa mikono ambao unalingana na mahitaji ya tasnia.

"Maabara hii inafungua uwezekano mpya wa kutoa masomo ya maingiliano, ya kujishughulisha, na ya vitendo ambapo Waalimu sasa wanaweza kufundisha na zana zinazoiga mazingira halisi ya muundo wa ulimwengu, kuwasaidia kujenga uwezo ambao soko la kazi la leo linahitaji."amesema Shin .

Amefafanua kuwa ,mradi huo unaboresha ustadi wa vitendo katika kubuni na utengenezaji wa 3D, na unawasaidia vijana wa Kitanzania kuwa na ushindani zaidi katika soko la kazi na kuwa tayari kwa kazi katika tasnia

zinazoendeshwa na uvumbuzi, tunakuza ujasiriamali, kuwapa wanafunzi nafasi ya kubuni, mfano, na hatimaye hata kuzindua bidhaa zao wenyewe.

### MATUKIO MBALIMBALI WAKATI WA WAZINDUA MAABARA YA UBUNIFU IDARA YA UHANDISI MITAMBO.










